



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI



MAOMBI YA USAJILI NA UKAGUZI WA MAJENGO YA KUTOLEA HUDUMA YA DAWA (FAMASI) KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI

Baraza la Famasi linapenda kuwatangazia Wakaguzi wote kwa ngazi ya Baraza, Mikoa na Halmashauri pamoja na wananchi wote kwa ujumla kuwa, idhini ya eneo la kuanzisha famasi (**Application for approval of location**), ukaguzi wa awali wa eneo na ukaguzi wa mwisho wa majengo (**First and Full Inspection**), usajili wa majengo (**Premises Registration**) na ukaguzi wa kawaida wa huduma za dawa (**Routine Inspection**) utaanza kufanyika rasmi kwa njia ya kielektroniki kuanzia tarehe 17 Februari, 2025 kwa utaratibu ufuatao:

1. Kila muombaji anayetaka kuanzisha kutoa huduma za dawa (Kufungua Famasi) atahitajika kujisajili kwa kufungua akaunti kwenye mfumo wa Baraza la Famasi (**PCMIS**) na kujaza taarifa zote muhimu zinazohitajika.
2. Mwombaji kujaza taarifa zote muhimu kuhusu eneo linaloombewa idhini na kulipa ada stahiki ya ukaguzi wa eneo husika.
3. Mwombaji kuhakikisha anatumia akaunti yake mara kwa mara kupitia na kufahamu mwenendo wa maombi yake na hatua za usajili wa jengo baada ya kukamilisha taratibu zote kama zilivyoainishwa kwenye kanuni za usajili wa majengo.
4. Wakaguzi kutumia Mfumo wa *PCMIS* kufanya kaguzi zote zinazohusu idhini ya eneo, usajili wa jengo na ufuatiliaji wa utoaji wa huduma za dawa katika majengo (Famasi) na kujaza taarifa zote muhimu kuanzia tarehe ya tangazo hili.
5. Kwa mawasiliano zaidi tafadhari wasiliana na Ofisi a Baraza kupitia mawasiliano yafuatayo:
 - (i) **Kanda ya Mashariki**- [Dar, Pwani, Lindi na Mtwara] **0736 222 523**
 - (ii) **Kanda ya Kaskazini** [Arusha, Manyara, K'njaro, Tanga] **0736 222 531**
 - (iii) **Kanda ya Kati** [Dodoma, Morogoro, Singida, Iringa] **0736 222 527**
 - (iv) **Kanda ya Magharibi** [Tabora, Katavi, Rukwa, Kigoma] **0736 043 602**
 - (v) **Kanda ya Ziwa** [Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Mara, Geita] **0736 222 501**
 - (vi) **Kanda ya Nyanda za juu Kusini** [Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe] **0739 222 537**
 - (vii) **Makao Makuu - Dodoma:** **0736 222 515**
 - (viii) **Kurugenzi ya Usajili, Maendeleo Taaluma na Utafiti:** **0736 222 503**
 - (ix) **Kurugenzi ya Utendaji wa Taaluma na Udhhibiti:** **0736 222 514**
 - (x) **Kitengo cha TEHAMA:** **0736 222 514**

NB: Bonyeza [hapa](#) kupata utaratibu wa namna ya kufungua akaunti na kuwasilisha maombi ya idhini ya eneo na usajili.

Imetolewa na:

Msajili, Baraza la Famasi

S.L.P. 1277, Dodoma

Simu: 0756710791/0800110015

Barua pepe: info@pc.go.tz / registration@pc.go.tz / inspection@pc.go.tz